# Tafsiri Tenge za Dhana Asilia za Kiswahili kwenye Lugha ya Kiingereza katika Vyombo vya Habari

*Ahmad Y. Sovu*
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere*

**Ikisiri**

**Vyombo vya habari ni asasi muhimu katika kufikisha ujumbe kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Vyombo hivyo ni televesheni, magazeti, idhaa za redio, mitandao ya kijamii n.k (Kambaya, 2022). Nyenzo kubwa itumiwayo na vyombo vya habari katika kuhakikisha ujumbe unafika kwa wakati na kwa ufasaha uliokusudiwa ni lugha. Hapa tunazungumzia lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, makala haya yanalenga kuonesha mtindo unaozidi kushamiri wa kufasiri dhana asilia za Kiswahili kwa kuegemea lugha ya Kiingereza, taathira zake na kutoa mazingatio muhimu kwa vyombo vya habari. Nadharia ya tafsiri iliongoza uchunguzi huu. Data zilikusanywa kwa njia ya maktabani kwa kupitia kwa umakini maandiko mbalimbali, ushuhuduaji na usaili. Matokeo yamedhihirisha kuwa kuna tafsiri za kiholela ambazo hufanywa haraka haraka zinazoweza kuingiza ruwaza tenge zenye ukakasi katika lugha ya Kiswahili. Mathalan, kusema mwisho wa siku kwa tafsiri ya *at the end of the day* badala ya hatimaye, Imebainika pia, kukithiri kwa utenge huu kunaweza kuleta athari ya kuwa na 'Kiswanglish'-yaani Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza au Kiswahili cha Kiingereza. Vilevile, makala inapendekeza mazingatio muhimu ya kuboresha mazao ya tafsiri katika vyombo vya habari kuwa ni; wafasiri katika vyombo vya habari wawe weledi,watumie istilahi sanifu za Kiswahili kwa kujiamini, waendeleze dhima ya kutangaza marekebisho ya tafsiri tenge za Kiswahili, washirikiane na wataalamu wafasiri kutoka vyombo vya ukuzaji wa Kiswahili na wasilazimishe kutafsiri dhana za utamaduni na mila za kigeni katika Kiswahili. Makala yanatoa mchango katika uga wa tafsiri na maendeleo ya Kiswahili.**

**Maneno Muhimu**: *Tafsiri Tenge, Dhana Asilia, Kiingereza, Vyombo vya Habari*

## Utangulizi

Vyombo vya habari ni asasi muhimu katika kufikisha ujumbe kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia usambazaji huo umekuwa ukifanywa ama kwa mitindo tofauti ili kuwafikia walengwa kwa wakati na ujumbe ufike kama ulivyokusudiwa. Kwa mujibu Mohochi kama alivyomnukuu (Harris, 1989) anasema vyombo vya habari vimegawanyika katika makundi mawili, kundi la *uchapishaji* na *utangazaji*. Kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia vyombo vya habari tunaweza kuongeza kundi la tatu ambalo ni *mitandao* (Mohochi,2006). Anaendelea kueleza kuwa, vyombo vya habari vya uchapishaji hujumuisha magazeti, majarida, n.k na hudhihirika katika maandishi. Vyombo vya habari vya utangazaji ni pamoja na redio, televisheni na sinema. Hivyo hudhihirika katika hali ya mazungumzo na picha. Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa sana wa kuathiri umma kwa sababu hupitisha ujumbe kwa hadhira pana sana, vyombo vya habari vya mtandao hudhihirika katika sura zote mbili, yaani huweka habari katika maandishi ya kieletroniki na huweka pia habari katika sauti. Mtandao una uwezo mkubwa zaidi wa kufikia hadhira ulimwenguni kote.

Idadi kubwa ya habari hizo chanzo chake ni shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na viongozi na watendaji wa kisiasa na kiserikali wa nchini vilimo vyombo vya habari husika. Hii ni pamoja na maagizo na maelekezo ya viongozi; kazi za ujenzi wa taifa za wananchi, michezo, semina, warsha, makongamano, mikutano ya kitaifa na mahubiri ya dini mbalimbali. Vyanzo hivi huwa aghalabu katika lugha ya taifa inayoeleweka na takribani na wananchi wote. Kwa upande wa Tanzania mathalan, lugha hiyo ni Kiswahili.

Pamoja na vyanzo hivyo vya habari, vipo pia vyanzo vya asasi za kimataifa vilivyomo nchini na vya kutoka nje ya nchi. Hivi kwa kawaida huwa katika lugha za kigeni na, hivyo, taarifa zake

hulazimika kutafsiriwa kwa lugha ya taifa kabla hazijatolewa kwa walaji, yaani kwa Tanzania, wananchi wazungumzaji wa Kiswahili. Kwa mazingira ya Tanzania, ambayo kwa kipindi kirefu ilitawaliwa na dola ya Uingereza iliyokuwa na será ya kukisimika barabara Kiingereza katika makoloni yake, Kiingereza ndiyo lugha chanzi (LC) kuu ya tafsiri ya Kiswahili.

Nyingi ya tarifa zilizotafsiriwa kwa Kiswahili tunazozipata kwenye vyombo vya habari nchini mwetu zinatokana na lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, kutokana na mbinu za tafsiri zinazotumika na pia weledi hafifu wa fani ya tafsiri miongoni mwa wafasiri wanaohudumu katika vyombo vya habari, baadhi ya tafsiri za Kiswahili katika vyombo hivi imebainika kuwa zinaeleka kukengeusha Kiswahili sanifu na fasaha. Kwa hakika tafsiri hizo ni tenge. Zinaendelea kutumika katika Kiswahili kwa kuvumiliwa tu, japo mashabiki wa tafsiri hizo hudai kukifanya Kiswahili kionekane cha kisasa kinachoenda na wakati.

Madhumuni ya makala haya ni kuonesha mtindo unaozidi kushamiri wa kufasiri dhana asilia za Kiswahili kwa kuegemea lugha ya Kiingereza, taathira zake na mapendekezo ya mazingatio muhimu kwa vyombo vya habari kuepuka hali hii.

Makala yamegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ambapo tumetoa maelezo mafupi kuhusu Kiswahili na vyombo vya habari, nadharia na methodolojia za ukusanyaji wa data. Sehemu ya pili na ya tatu ni kiini, katika kiini tumejadili mbinu za kutafsiri, utenge na taathira. Sehemu ya tatu, imeonesha mapendekezo ya mazingatio muhimu kwa vyombo vya habari kupunguza au kuondoa hali hiyo na tano ni hitimisho.

**Vyombo vya Habari na Lugha ya Kiswahili**

Kulingana na Mohochi, (2006) Lugha ya Kiswahili inanufaika sana kutokana na jukumu muhimu linalotekelezwa na vyombo vya Habari katika harakati za kuikuza, kuiendeleza na kuisambaza. Akimnukuu Dadi (1995). Mohochi (keshatajwa) anasema:

> …Hapa Afrika Mashariki na Kati vyombo vya habari viko katika mstari wa mbele kuendeleza lugha hii ambapo vipindi vya redio na televisheni vinasikika kila siku.

Yaelekea kuwa ni jambo linalokubalika kwa wengi kwamba vyombo vya habari vimetoa mchango mkubwa kuikuza lugha ya Kiswahili. Lakini tukumbuke, kama anavyotutanabaisha Kinganya (1995), kwamba vyombo vya habari vina uwezo wa kukwamisha au hata kupotosha lugha inayohusika. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kuzingatia hadhari katika matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, pamoja na kazi nzuri za vyombo vya habari katika kukuza na kuendeleza Kiswahili, yapo makosa kadhaa yanayodhihirika katika matumizi ya vyombo hivyo vya habari. Shabaha ya makala haya si kuchunguza makosa hayo ya moja kwa moja. Bali ni kuchunguza baadhi ya tafsiri za Kiswahili katika vyombo hivyo zinavyoegemezwa katika Kiingereza na kutumika katika Kiswahili.

**Nadharia ya Tafsiri**

Nadharia ya tafsiri ni jumla ya maarifa yaliyopo na yanayopatikana kuhusu mchakato wa kufasiri, kuanzia misingi na kanuni za jumla za mwongozo, mapendekezo na vidokezo muhimu (Mwansoko, 2006). Katika nadharia hii moja ya jambo linaloshughulikiwa ni kupendekeza taratibu zinazofaa zaidi kutekeleza zoezi la kufasiri pamoja na mbinu mwafaka zaidi kwa matini mahsusi inayoshughulikiwa. Hivyo, nadharia hii imetumiwa ili kusaidia wafasiri katika vyombo vya habari wafanye uteuzi mzuri wa kile kinachofaa.

**Methodolojia ya Utafiti**

Data za msingi kwa ajili ya makala haya zilipatikana kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa nyaraka ya kusoma kwa makini baadhi ya maandiko yanahusiana na mada hii. Uchambuzi wa nyaraka kama wasemavyo Ngesu na Mrikaria (2022), ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo kwayo mtafiti husoma matini, kuzichambua na kuzichanganua ili kupata data kulingana na malengo ya utafiti. Ngesu na Mrikaria (weshatajwa), wakimnukuu Riaz (2018) na Khan (2019) kwamba, uchambuzi wa nyaraka ni mbinu inayotumiwa kukusanya data na taarifa kutoka kwenye maandishi mbalimbali ambayo yamechapishwa au ambayo hayajachapishwa. Katika makala haya matini au maandiko

kuhusu wataalamu mahiri wa tafsiri waliochunguza kasoro kadhaa za tafsiri kama vile; Mwansoko, Mekacha, Masoko, Mtesigwa na Fupi vilipitiwa kwa utondoti. Aidha, data nyingine katika makala haya zilipatikana kwa kutumia njia ya ushuhudiaji na usaili na kubaini tafsiri tenge zilizofasiriwa na baadhi ya vyombo vya habari kwa haraka haraka bila kuzingatia taratibu husika. Mbinu ya usaili ilitumika kwa kuwahoji wataalamu wa tafsiri ili kupata njia nzuri za kuondokana na hali hii. Data za usaili zilisaidia sana katika sehemu ya nne ya makala haya.

**Mbinu za Kutafsiri**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, (1.0) mbinu inayotumika kufasiri matini chanzi (MC) huathiri sana matokeo ya matini lengwa (ML) inayozalishwa. Hivyo, ni muhimu sana tukabainisha hapa mbinu zinazotumiwa kufasiri matini za Kiingereza kwenda katika lugha yetu ya Kiswahili. Zipo mbinu au njia mbalimbali za kutafsiri. Newmark (1988), kwa mfano, ametaja mbinu 13; Mshindo (2010:133-142) ametaja mbinu nane; na Mwansoko (1996) na Wanjala (2011:67-74) wamebainisha mbinu nne.

Hata hivyo, utendaji halisi wa kazi za kutafsiri umeonesha kuwa ni mbinu mbili (2) tu za kutafsiri zilizo na mdafao mkubwa, yaani tafsiri ya kimawasiliano (tafsiri huru) na tafsiri ya kisemantiki (tafsiri ya wazi). Wafasiri wengi hupendelea kuzitumia mbinu hizi kwa vile ndizo zinazotoa taarifa za kifasiri kwa usahihi zaidi na kwa kuzingatia uwekevu na iktisadi ya lugha. Hapa chini tunazifafanua mbinu hizo.

**Tafsiri ya Kimawasiliano**

Hii ni tafsiri ambayo humlenga msomaji wa ML ikijimili kumfikishia kwa kuzingatia sarufi, historia, mazingira, muktadha na utamaduni wake. Kwa dhati yake tafsiri ya aina hii humjali zaidi msomaji anayelengwa. Kwa kutumia mbinu hii ya kufasiri, mfasiri yupo huru kutafuta maneno au vifungu vya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, utamaduni na mazingira ya lugha lengwa (LL). Hivyo, tafsiri ya kimawasiliano hulenga kuhawilisha na kuibua athari ile ile ya MC katika ML. Mbinu hii hutumika zaidi kufasiri matini arifu (k.m. sayansi na teknolojia) na matini amili (k.v. matangazo, maombi, mialiko, propaganda).

**Mifano:**

*Like father like son* - rupia kwa nyenzie; mtoto wa nyoka ni nyoka

*No need to cry over* spilt milk- Maji yakimwagika hayazoleki

*Things Fall Apart* - Shujaa Okonkwa (Riwaya ya Chinua Achebe wa Nigeria)

*Knock at the door* - bisha;piga hodi *The Beautiful Ones are not yet bo*rn - *Wema Hawajazaliwa* (Riwaya ya Kwei Armah wa Ghana)

**Tafsiri ya Kisemantiki**

Aina hii ya tafsiri huegemea zaidi kwenye lugha chanzi (LC), ikijikita katika kufafanua kinagaubaga maana iliyokusudiwa na mwandishi wa LC. Hapa mfasiri hufasiri kila kipashio au kila neno katika MC kama lilivyo na kwa maana yake ya msingi lakini kwa kuzingatia kanuni za kisarufi na muktadha wa lugha lengwa (LL). Utaratibu huu wa kufasiri kwa neno mahsusi kila dhana, kipashio au neno la MC kwenda katika ML umesababisha miundo ya misemo ya LC kuhamishiwa kwenye LL na, hivyo, kuikuza ama kuiendeleza kwa namna fulani, hasa pale miundo hiyo ya misemo inapoingia polepole au taratibu katika LL. Lugha ya Kiswahili imefaidika kwa kiwango kikubwa kwa utaratibu huu ambapo miundo ya misemo kadhaa ya Kiingereza imeingia katika Kiswahili na kupanua ruwaza yake ya Kisarufi.

**Mifano**:

| | |
|---|---|
| In the name of Jesus Christ | -Katika jina la Yesu Kristo |
| In the name of Allah | -Kwa jina la Allah |
| The law shall take its own course | - sheria itafuata mkondo wake |
| Take the law in one's hands | -Jichukulie sheria mkononi |
| Ladies and gentlemen | -Mabibi na Mabwana |
| All the best | -Kila la Kheri |

Miundo iliyooneshwa hapo juu, kwa mujibu wa maoni yetu, imeitajirisha lugha ya Kiswahili na kuifanya ipanue ruwaza yake ya kisarufi. Wazungumzaji kindakindaki wa Kiswahili hawaonekani kukerwa nayo (kwa maana kuwa wanaikubali miundo hiyo), hivyo tunaweza kudiriki kusema kwamba huu ni mchango chanya wa tafsiri ya kisemantiki katika Kiswahili.

**Utenge wa baadhi ya Matini Zilizotafsiriwa Kisemantiki**

Kama ilivyobainishwa hapo juu kuwa tafsiri za kisemantiki zikiingia kwenye lugha pokezi taratibu, bila kulazimishwa, huwa polepole zinazoelewa na wazungumzaji wa lugha hiyo na, hivyo, kukubaliwa.

Lakini pale tafsiri hizo zinapoingizwa katika lugha pokezi kwa kasi, haraka, na pengine na wafasiri wasio na weledi wa fani ya tafsiri, basi aghalabu tafsiri hizo kuwa na ukakasi mkubwa na, hivyo, kuwatatiza wapenzi wengine wa Kiswahili sanifu na fasaha.

Mathalan, katika kipindi cha hivi karibuni, kutokana na maendeleo ya kasi ya teknolojia ya upashanaji habari, athari za utandawazi na shauku wa watu (wakiwamo wafasiri) kutaka kuonekana "wanakwenda kwa wakati" na wana raghba ya kukifanya Kiswahili kuwa cha kisasa, kumeanza kujitokeza kwenye vyombo vya habari, unenaji wa Kiswahili kwa maana ya Kiingereza kilichotafsiriwa kisemantiki. Yaani zinaibuliwa semi au tungo ambazo japo zinasikika kama Kiswahili lakini kwa dhati yake ni Kiingereza. Ni kama "Kiswaglish" cha aina yake. Kiswahili cha namna hii aghalabu hakifuati misingi ya utamaduni wala mazingira na itikadi ya lugha ya Kiswahili. Hapa chini katika jedwali namba 1 tunabainisha mifano michache ya tafsiri madhkura.

**Jedwali Namba 1. Baadhi ya Tafsiri Tenge za Kisemantiki katika Vyombo vya Habari**

| | |
|---|---|
| *At the end of the day* | Mwisho wa siku (badala ya 'hatimaye') |
| *The exercise of voting* | Zoezi la kupiga kura (badala ya 'shughuli ya kupiga kura') |
| *The first ebola case* | Kesi ya kwanza ya ebola (badaka ya 'tukio la kwanza la ebola) |
| *Think out of the box* | Fikiri nje ya boksi (badala ya 'fikiri vinginevyo) |
| *Rush the patient to hospital* | Kimbiza mgonjwa hospitalini (badala ya 'peleka mgonjwa haraka hospitalini). Hili ni tatizo la muda mrefu, kwani kinachoashiriwa hapa ni kinyume cha jambo linalotarajiwa litendwe, yaani "kumtoa mgonjwa nduki toka hospitali" |
| *To recognize the presence of* | Kutambua uwepo wa (badala ya 'kutambulisha kuwapo kwa mtu falani) |
| *Last but not least* | Mwisho lakini si kwa umuhimu (badala ya 'mwisho kabisa) |
| *My days are numbered* | Siku zangu zimehesabiwa (badala ya ''muda wangu umeisha') |
| *From the bottom of my heart* | Kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu (badala ya 'kwa dhati kabisa') |
| *Many cases of COVID-19* | Kesi nyingi za UVIKO-19 (badala ya matukio mengi ya UVIKO-19) |
| *Central Police Station* | Kituo cha Kati cha Polisi (badala ya Kituo Kikuu cha Polisi) Tatizo hili lilibainisha tangu zamani zaidi ya miongo miwili iliyopita, lakini hadi leo lingali likiendelea kutumika katika baadhi ya vyombo vya habari. |
| *Lead to; result into* | pelekea (badala ya 'sababisha') |

Matini za Kiswahili zilizobainishwa kwenye jedwali hapo juu, zinatokana na tafsiri za kisemantiki, kwa dhati yake ni tenge. Wapenzi kindakindaki wa Kiswahili sanifu na fasaha wanazivumilia tu, tena kwa uchungu.

**Taathira katika Tafsiri Tenge**

Ufasiri huu wa Kiswahili kwa kuegemea lugha ya Kiingereza na unafanana na kile kilichoitwa miaka 1989/90 "Kiswanglish"-yaani Kiswahili kilichochanganyikana na Kiingereza. Hiki si Kiswahili sanifu, fasaha na mwanana. Wakuzaji wa lugha ya Kiswahili watakuwa wanajidanganya endapo watadhani Kiswahili kinakuzwa na kustawishwa kwa miundo inayotokana na tafsiri za kisemantiki. (Tazama Mwansoko, 2016). Aliwahi kuulinganisha ukuzaji wa namna hii ya Kiswahili kama "mtu anayepiga hatua moja mbele, mbili nyuma!"

Athari hii inakuwa mbaya zaidi, kwani utenge huu wa Kiswahili unaathiri sana nchini Tanzania ambapo panachukuliwa kuwa kitovu cha Kiswahili sanifu na fasaha. Wakati wazungumzaji wenzetu wa Kiswahili waliopo ughaibuni, wanajifunza Kiswahili sanifu kama inavyoelekezwa na vitabu rasmi vya kiada na ziada, wanakiimarisha Kiswahili sanifu, sisi wamiliki wa lulu hii, tunaiharibu kwa makusudi. Matokeo yake ni kwamba siku za usoni Kiswahili mwanana kitaptikana zaidi ugenini kama vile China, Uingereza, Marekani, Ujerumani, Korea Kusini, Afrika Kusini, Namibia, badala ya Tanzania na Kenya ambako ndio masikani yake hasa. Hivyo, uholela wa tafsiri za kisemantiki katika Kiswahili hauwezi kuachwa uendelee na kushamiri. Kuna haja udhibitiwe ili kutoa fursa kwa dhana asilia za Kiswahili kuendelea kutamalaki.

**Mapendekezo ya Mazingatio Muhimu**

Ili tafsiri hizo ziwe fanikivu zaidi hapana budi zifanywe kwa kiwango cha juu cha ufanisi. Watoa tarifa walitoa maoni yao na kupendekeza mazingatio anuwai ya kuboresha mazao bora ya tafsiri katika vyombo vyetu vya habari. Mazingatio hayo ni pamoja na haya yafuatayo:

**Wafasiri katika Vyombo vya Habari wawe Weledi**

Alisema mmoja ya mtoa tarifa ambaye ni mtaalamu wa taaluma ya tafsiri.

> …Tafsiri, yaani ule mchakato wa uhawilishaji ujumbe, maarifa au tarifa katika maandishi kutoka matini chanzi (MC) kwenda matini lengwa (ML) kwa kuzingatia isimu, utamaduni na muktadha wa jamii lengwa, ni taaluma au fani mahsusi. Fani hii ina nadharia, kanuni, mbinu na kaida au taratibu zake, ambazo wafasiri hawana budi kuzimaizi, tena kwa utondoti.

Maelezo haya ni ya muhimu. Hivyo, ili mfasiri awe fanikivu katika kazi yake, hana budi aifahamu vema taaluma ya tafsiri. Kuwa na ujuzi na umilisi wa lugha mbili au zaidi si kigezo tosha cha mtu kuhudumu kama mfasiri. Utafiti wa muongo uliopita ( taz. Kwa mfano Mutasa 1999; Walibora 2001; Fupi 2010; Emanuel 2011) ulibainisha kuwa wafasiri wengi walioajiriwa katika vyombo vya habari hawakuwa na weledi wa fani ya tafsiri. Hali hii haijabadilika hadi sasa. Wamiliki wa vyombo vya habari huchukulia kuwa mtu yeyote anayejua Kiswahili na Kiingereza walau kwa kiwango cha Chuo Kikuu anao uwezo wa kufasiri katika lugha hizo. Ukweli ni kwamba, imani hii tumebaini kuwa ni potofu na inaendelea kusababisha kuwapo kwa utenge katika baadhi ya tarifa zinazotokana na tafsiri na kutangazwa katika vyombo vya habari.

**Wafasiri Wazitumie kwa Kujiamini Istilahi Sanifu za Kiswahili**

Kwamba Kiswahilli ni lugha kubwa-kitaifa, kikanda na kimataifa ni jambo lililo dhahiri (taz.Mwansoko, 2021). Hivi sasa yakaribia karne moja tangu Kiswahili kilipoanza kukuzwa na kuendelezwa kwa ajili ya matumizi katika maeneo rasmi ya kiserikali kama vile kufundisha shuleni, mawasiliano ya kisiasa na kiutawala na pia mawasiliano kupitia vyombo vya habari. Lugha kuwa imetumika katika mawasiliano mapana rasmi kwa kipindi kirefu namna hii (yaani zaidi ya miaka mia moja) ni uthibitisho wa ubora na uimara wa lugha hiyo. Wazungumzaji wa lugha hiyo hawapashwi kuwa na wasiwasi ama tashwishi wanapoitumia, bali wajiamini na kiamini lugha yao. Dhana ya "kujiamini" hapa inamaanisha kuwa na moyo wa kutokuwa na shaka na uwezo wa jambo au kitu fulani unachodhamiria kukifanya (taz, KKS 2014; KKK 2017).

Anafafanua ndugu Champunga kama mtoa tarifa na mtaalamu wa lugha kuwa;

> …Katika makuzi ya muda mrefu ya lugha ya Kiswahili, kumebuniwa istilahi (yaani msamiati maalumu wa nyanja anuwai za maarifa) kwa kufuata misingi na kanuni za kimataifa za uundaji wa istilahi. Istilahi

> hizo hizo zimesanifishwa na asasi za kiserikali zenye wajibati na mamlaka hayo. (k.v. BAKITA, BAKIZA, TATAKI) na, hivyo, hazina budi kutumiwa zilivyo pasi na wasiwasi na bila kuhitaji kuwekewa visawe vyake vya Kiingereza.

Mifano michache kama hapa chini kama ilivyonukuliwa kutoka vyombo vyetu vya habari inadhihirisha hilo kama lilivyofafanuliwa na mtoa taarifa;

- Uchunguzi wa awali, yaani 'screening' (Habari ITV, 27/01/2022)
- Sampuli kifani, yaani "proto type" (Habari, Channel Ten, 16/02/2022)
- Mshituko wa moyo (cardiac arrest). Hili lilijitokeza katika magazeti mengi kufuatia kifo cha Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Tanzania, Benjamin William Mkapa, tarehe 23, Julai, 2020.

Ufafanuzi wa namna hii wa istilahi za Kiswahili hauna sababu zozote za msingi, bali unaonesha kutojiamini kwa wafasiri na pia unaashiria kutokuaminika kwa istilahi zenyewe za Kiswahili. Hali hii sio nzuri kwa mustakabali wa lugha yetu adhimu ya Kiswahili.

**Vyombo vya Habari Viendeleze Dhima ya Kutangaza Marekebisho ya Tafsiri Tenge za Kiswahili**

Ni jambo lisilopingika kwamba wasikilizaji, wasomaji na hata watazamaji wa vyombo vya habari huviamini sana vyombo hivyo kuwa ni vyanzo madhubuti vya taarifa na maarifa mbalimbali. Kwa maneno mengine, vyombo vya habari ni shule; ni kisima panapochotwa elimu na utaalamu anuwai (Eliah, 2019). Imebainishwa kuwa, eneo moja ambalo limefaidika sana na kuwapo kwa vyombo vya habari na kuziondosha matumizini istilahi zilizokuwa zimekosewa awali na badala yake kuzitangaza istilahi sahihi zilizobuniwa upya na wanaistalahi wa Kiswahili. Dhana za kigeni zinapotafsiriwa na kupewa viwakilishi vya kiistilahi vya Kiswahili na kisha kutangazwa kupitia vyombo vya habari, umma huzipokea kwa kuamini kuwa zi sahihi. Kumbe pengine huwa zimekosewa, si kwa makusudi bali kwa upungufu tu wa kibinadamu. Makosa yakibainishwa hurekebishwa, na ndipo hapo vyombo vya habari husaidia sana kutangaza marekebisho ya zilizokuwa tafsiri tenge za Kiswahili. Tutazame mifano ifuatayo:

| **Istilahi tenge** | **Istilahi Sahihi** | **Matini chanzi ya Kiingereza** |
|---|---|---|
| King'amuzi | kisimbuzi | decoder |
| Mauaji ya halaiki | mauaji ya kimbari | genocide |
| Mrahaba | mrabaha | royalty |
| Mgeni wa heshima | mgeni rasmi | guest of honour |
| Waziri asiye na Wizara Maalum | Waziri- Kazi Maalum | Minister without Potfolio. |

Bila kuwapo usaidizi mkubwa wa vyombo vya habari, istilahi sahihi zilizorejelewa hapo juu zisingepata mashiko katika Kiswahili. Lugha ingeendelea kubanangwa kwa kutumia istilahi tenge.

Mwito uliotolewa na watotarifa katika utafiti huu ni kuwa harakati hizo za kutangaza istilahi sahihi za Kiswahili mahali pa zile zilizo tenge kupitia vyombo vya habari ziendelee. Baadhi ya istilahi (semi) tenge zilizo matumizini nazo zinapaswa kurekebishwa ni pamoja na:

- Ufaulu (badala ya 'kufaulu'
- Mtambuka (badala ya 'mtambuko')
- Manunuzi (badala ya 'ununuzi'). Hapa tunaweza kuongeza pia: mashirikiano, mahusiano, mapungufu.
- Hairisha (badala ya 'ahirisha')
- Dijitali (badala ya 'dijiti')
- Kidijitali (badala ya 'kidijiti')
- Kwa jina (majina) naitwa (badala ya 'jina langu ni…')
- Mbeleni (badala ya 'mbele/siku za usoni')

**Baadhi ya Dhana za Utamaduni na Mila za Kigeni si lazima Zitafsiriwe kwa Kiswahili**

Wakati mwingine watenda kazi wa habari hukutana na dhana za kiutamaduni katika marejeo yao ya matini za lugha za kigeni kama vile Kiingereza au Kifaransa. Endapo dhana hizo hazina uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni wa Kiswahili. (na hata na tamaduni zingine za Kibantu) wafasiri katika vyombo vya habari wasijilazimishe kufasiri, au kufasiriwa, matokeo yake hayakuwa fanikivu. Imebainika kuwa zilijitokea tafsiri zilizosheheni ukakasi. Tazama mifano ifuatayo:

- First lady (mgoli?)
- Birthday (mazazi? Siku ya mazazi? Sabukuu?)
- Chopstick (chopstiki)
- Bon-appetite (karibu?)
- Eggchop (yainyama)

Dhana za namna hii, ambazo wala si muhimu sana katika mila na desturi za Kiswahili, zisipotafsiriwa hazitaleta madhila yoyote. Ikilazimika sana ziingizwe katika Kiswahili. Basi mbinu ya utohozi inaweza kutumika.

**Wafasiri wa Habari Washirikiane na Wafasiri Weledi aliopo katika Vyombo Mbalimbali vya Kiswahili**

Imeshauriwa kuwa ili kuepuka tafsiri holela za kisemantiki na kuepuka kuingiza tafsiri tenge au zenye ukakasi katika lugha sanifu na fasaha. Wafasiri wa vyombo vya habari ni muhimu wafanye kazi kwa karibu na wataalamu weledi katika vyombo ambavyo vinahusika na maendeleo ya Kiswahili. Mathalan, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) na idara za lugha za Kiswahili katika vyuo vikuu mbalimbali katika nchi hususan za Kenya na Tanzania. Ushirikiano huu, utakuwa wa kitaalamu na kiuweledi. Ambapo ikiwa kuna maneno au semi fulani zinatakiwa kufasiriwa kwa Kiswahili basi wataalamu wa fani hizo wanaweza kushirikiana na kupata tafsiri ambazo zitakuwa faafu zaidi.

**Hitimisho**

Kwa kuwa tafsiri ni mojawapo ya vichocheo vya makuzi na ustawishaji wa lugha inapotumiwa kwa weledi. Hivyo, madhumuni ya makala haya yalikuwa ni kuchunguza dhima kubwa ya tafsiri ya kisemantiki katika kuendeleza na kukuza lugha pokezi ya tafsiri, aina hii ya tafsiri ikitumika kiholela inaweza kuingiza ruwaza tenge au zenye ukakasi katika lugha fasaha na sanifu. Hali hiyo imebainishwa katika makala haya. Pia, makala yamebainisha hali ya taathira ambazo zinaweza kujitokeza kwa kufanya tafsiri hizo.Ambazo ni kuibuka 'Kiswanglish', yaani Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza, kupokwa kwa uweledi wa Kiswahili sanifu kwa nchi za Tanzania na Kenya ambazo huchukuliwa kuwa ndio kwao na Kiswahili. Badala yake wataalamu na wafasiri wazuri wanaweza kuibuka katika nchi nyingine za ughaibuni.

Vilevile, makala yamependekeza mazingatio ya uboreshaji wa ufanisi wa tafsiri zinazojitokeza katika vyombo vya habari vinavyotumia lugha ya Kiswahili**.** Ili tafsiri katika vyombo hivyo ziwe fanikivu zaidi imependekzwa wafasiri wawe weledi katika kazi zao za tafasiri na tafsiri ya dhana asilia za Kiswahili kwa kuegemea kwenye lugha ya Kiingereza uepukwe kila itakavyowezekana. Aidha, tumehimiza wafasiri waziamini istilahi za Kiswahili zilizosanifiwa na wazitumie bila kuziweka sambamba na visawe vyake vya Kiingereza. Zaidi ya hapo, vyombo vya habari vinahimizwa kuwa jukwaa la kutangaza marekibisho ya tafsiri tenge za Kiswahili ili istilahi sahihi zitambulike na kukita mizizi matumizini. Fauka ya hayo, imehimizwa wafasiri katika vyombo vya habari kushirikiana na wataalamu weledi wa kutafsiri kutoka katika taasisi zinashughulika na ukuzaji wa Kiswahili na vyuo vikuu ili kupata tafsiri faafu zisizokuwa na ukakasi wala utenge.

Mwisho, limetolewa pendelekzo kwamba dhana za utamaduni wa kigeni ambazo sio muhimu sana katika mila na desturi za Kiswahili, yaani hazina uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni wa Kiswahili, zisilazimishwe kufasiriwa kwa Kiswahili.

**Marejeo**

BAKITA, (2029). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Nairobi, Longhorn Publishers Ltd.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Eliah.V. (2019). *Kiswahili katika Vyombo vya Habari: Ndani na Nje ya Tanzania*, Dar es Salaam, TATAKI.

Dadi, K. S. (1995). "Dhima ya Vyombo vya Habari katika Matumizi ya Msamiati", katika Mlacha (Mh.) *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: TUKI.

Emmanuel, E. O. (2011). "The Impact of Pragmatic Competence in Traslation: The case of BBC English Kiswahili World News Traslations", Tasinifu ya Umahiri,(Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Fupi, R. (2010). "A Critique of Electronic Media Tranlations: A Case Study of TBC (Television) English Swahili News Translations", Tasinifu ya Umahiri, (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jilala, H. (2014) "Athari za Kitamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania". Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Harris, R.J. (1989). *A Cognitive Psychology of Mass Communication,* Lawrence New Jersey. London. Earlbaum Associates Publishers.

Kambaya, M. (2022). "Nafasi ya Redio katika Kujenga Umoja wa Afrika kupitia Lugha ya Kiswahili: Uzoefu wa Redio One" katika *Kiswahili katika Anga za Kimataifa, Julai 7, Siku ya Kiswahili Duniani.* (Mtesigwa P. na Duwe. E) (Wah.) Dar es Salaam: TUKI na BAKITA.

Kiganya, W. (1995). "Sera ya Kiswahili, Mafanikio na Matatizo Nchini Kenya", katika Mlacha Mh.) *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki*. Dar es Salaam:TUKI.

Kiango, J.G. (2008). *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Khan, N. I. (2019). Case Study as a Method of Qualitative Research. *Qualitative Techniques for workplace Data Analysis* (kur.170-196). IGI Global. Inapatikana katika http://www.igi-global.com/chapter/case-study-as-a-method-of-qualitative-research/207797. Ilisomwa tarehe 15/2/2019.

Makunja, G. S. (1995). "Sarufi na Msamiati wa Kiswahili katika Vyombo vya Habari", katika Mlacha (mh.) *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam:TUKI.

Mohochi, E. S. (2006). "Kiswahili na Vyombo vya Habari nchini Kenya: Makosa katika Matumizi ya Lugha" katika *Kiswahili*. Juz 69. (Massamba, D.P.B) (Mh) Dar es Salaam: TUKI.

Mrikaria, G. na Ngesu, S.N. (2022). "Tafsiri kama Nyenzo ya Kutandawaza Utamaduni wa Mswahili: Mfano wa *Siku njema* (1996) na *A Good Day* (2019) katika *Kiswahili*. Juz 85 (2) (Mnenuka na Mpemba) (Wah.) Dar es Salaam. TUKI.

Mwansoko, H. J. M. (2021) *Misingi ya Kukuza Kiswahili Kimataifa*, Mhadhara wa Uzinduzi wa Uprofesa, Mbeya, Chuo Kikuu Teofilo Kisanji.

Mwansoko, H. J. M., Mekacha, R.D.K., Masoko, D.L.W. na Mtesigwa, P.C.K (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mwansoko, H. J. M. (1995). "Dhima ya Vyombo vya Habari katika Ukuzaji, Usanifishaji na Uenezaji wa Istilahi", katika, Mlacha (mh.) *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: TUKI.

Riazi, A.M. (2018). "Mixed Methods Approaches to Studying Second Language Writing". *The TESOS Encyclopaedia of English Language Teaching*, kur.1-6.

TATAKI, (2014) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press: Nairobi.

Waliibora, K.W (2001) "Matatizo ya Taarifa katika Vyombo vya Habari" katika *Kiswahili,* Dar es Salaam, TUKI, Juz.64:23-30.

Vituo vya Televisheni na Magazeti Mbalimbali.